

KILELE CHA MAADHIMISHO YA CCT DAY KWA MWAKA 2023

Katika Halmashauri Kuu na Mkutano Mkuu wa CCT wa mwaka 2021 uliridhia kubadili siku ya Maadhimisho ya Siku ya CCT (CCT Day) kutoka jumapili ya tatu ya Januari kila mwaka na kuadhimishwa mwezi wa tano na kilele chake kuwa Jumapili ya mwisho ya Mwezi Mei kila mwaka. Kwa mwaka 2023 Kilele cha Maadhimisho ya CCT Day imepangwa kuwa Jumapili tarehe 28 Mei Mkoani Kilimanjaro.

Lengo la maadhimisho ya CCT Day ni **kudumisha Umoja wa CCT na kuitegemeza CCT katika utoaji wa huduma za kitume na kijamii.**

Kichwa cha Neno la Mungu kitakachotumika kwenye maadhimisho ya CCT na kwenye mikutano yote ya CCT kwa mwaka 2023 ni “1 Kor. 3:1-12

“...Kulijenga Kanisa katika msingi wa Yesu Kristo...”